

TANGAZO NDUGU WANANCHI

MKURUGENZI WA MANISPAA YA LINDI ANAWATANGAZIA WANANCHI KUWA:

TASAF makao makuu kwa kushirikiana na Hamashauri ya Manispaa ya Lindi itafanya uhakiki na uhuishaji wa taarifa za walengwa katika mitaa yote 30 iliyopo kwenye Mpango. Zoezi hili litafanyika kwa muda wa siku moja katika vituo vya malipo.

Hivyo, wawakilishi wa Kaya wote wanatakiwa kufika eneo lililopangwa kwa ajili ya uhakiki kuanzia saa mbili Asubuhi na kuzingatia yafuatayo:

1. Mwakilishi wa kaya ambaye ndiye anapokea ruzuku afike na vitambulisho vifuatavyo;
 - Kitambulisho cha **Taifa (NIDA)** au namba ya **NIDA**,
 - Kitambulisho cha **mpiga kura**,
 - Kitambulisho cha **TASAF** au risiti yoyote ya malipo
 - Mwakilishi wa kaya ambaye hatakuwa na vitambulisho vilivyotajwa afike na barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Mtaa anaoishi.
 - Mwakilishi wa kaya pia anatakiwa afike na taarifa zake na wanakaya anaoishi nao.
2. Kwa kaya zenye watoto wa umri wa miaka 0-5 waje na kadi za kliniki kwa kila mtoto.
3. Kwa kaya zenye watoto ambao wako shuleni waje na Daftari la mtoto la shule lenye jina kamili la mtoto, shule na darasa analosoma kwa kila mtoto.

Zoezi la uhakiki ni muhimu kwani, **kaya isiyohakikiwa itakuwa imejitoa yenyewe katika mpango.**